JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

Simu: +255262963470
Nukushi: +255262963117
Barua pepe: ps@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz

Mji wa Serikali,
Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S. L. P 2996,
**DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

**DODOMA – 27 MACHI, 2020**

Mheshimiwa Innocent L. Bashungwa, Waziri wa Viwanda na Biashara amepiga marufuku uuzaji wa **Ethanol** nje ya nchi. Hatua hii inalenga kuimarisha upatikanaji wa malighafi hiyo nchini ili kuviwezesha viwanda vya ndani kuzalisha kwa wingi vitakasa mikono. Hii itasaidia kukabiliana na mahitaji makubwa ya bidhaa hiyo ndani ya nchi.

Aidha, Mheshimiwa Waziri amewataka wenye viwanda vinavyozalisha *Ethanol* kuongeza uzalishaji ili kuhakikisha *Ethanol* inapatikana kwa wepesi hasa kwa kipindi hiki ambacho nchi inapambana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID- 19).

Zuio hili litaanza kutekelezwa kuanzia tarehe 27 Machi, 2020.

Imetolewa na:

Prof. Riziki S. Shemdoe
**KATIBU MKUU**